**“Umuhimu Imewekwa Juu Yangu”**

**(“Necessity Is Laid Upon Me”)**

**Na**

**Alex Sadat**

**“Umuhimu Imewekwa Juu Yangu”**

**Na**

**Alex Sadat**

**Juni 26, 2021**

# “Umuhimu Imewekwa Juu Yangu”

Tunajisikiaje kuhusu kazi ya injili ambayo Mungu ametupatia kufanya? Je tunaiona kama mzigo? Au tunaichukulia kama nafasi? Hisia za Paulo zinaweza kutusaidia kustawisha majibu sahihi ya kazi zetu. Paulo aliandika, “*Maana ijapokuwa naihubiri injili sina la kujisifia maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri injili! Maana nikitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu; ila ikiwa si kwa hiari yangu, nimeaminiwa uwakili. Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa nihubiripo, nitaitoa injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika injili. Maana ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifaanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi, kwa wale walio chini ya sheria nalikuwa kama chini ya sheria, ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria, ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wassio nasheria naalikuwa kama sina sheria, si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo, ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu.*” (1 Kor. 9:16-22).

Paulo mara nyingi alipenda roho za watu. Alitaka kuona wengi wakiokolewa ikiwezekana. Hiyo ikiwa ni himizo lake, Paulo hakuona kazi yake kama inayochosha au inayoudhi. Kinyume, Paulo alihisi kuwa na wajibu mkubwa na kutaamani kuhubiri injili ya Kristo. Kwa shauku yake kwa ajili ya roho, Paulo alichukua muda kujifunza kuhusu wasikilizaji wake kwa mahubiri. Kama alikuwa anahubiria kundi ambalo kimsingi walikuwa Wayahudi, basi Paulo angeweza kuhubiri kwa namna ambayo Wayahudi wangelipokea. Vivyo hivyo, kama Paulo angekuwa anafanya kazi na wale “wasio na sheria”, basi Paulo angeweza kunena nao vizuri pia.

Kwetu sisi. Mungu ametupatia majukumu ya kuhubiri injili iyo hiyo! Ambayo Paulo alihubiri. “*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.*” (Marko 16:15-16). Kwanza kabisa, je tunahisi kama kuwa na wajibu kama huo kutimiza wajibu wetu kama Paulo alivyofanya? Je tunapaswa

kuahidi “ole” juu yetu wenyewe kama tusingekuwa watendaji? Tunapaswa kukumbuka kwamba wajibu wetu wa msingi ni ile ya kuwa Wakristo waaminifu (Efe. 4:1). Kama sitimizi wajibu wangu kwa sasa ipasavyo basi napaswa kufanya liwezekanalo ili nirudi katika kazi. Tunaishi katika ulimwengu ulio na watu bilioni 7.5 (hiyo ni bilioni ikiwa na neno “b”)! Miongoni mwatu hawa nimewahubiria wangapi injili? Hapana, hapana, hapana! Sizungumzii kuhusu kuwakaribisha kwenye ibada zetu.  nimewafundisha wangapi injili ya Yesu Kristo? Je idadi iko chini? Je tunaona haya kukubali kwamba idadi hiyo ni ya chini? Siku za awali, roho nyingi zinaingia katika umilele na kupotea katika dhambi zao. Nahitaji kuhisi umuhimu wa “kuokoa baadhi” kama Paulo alivyofanya (1 Kor. 9:22). Hiyo inamanisha kwamba naitaji kujiingiza katika maisha ya majirani zetu. Hiyo pia inamanisha kwamba napaswa kujiingiza katika maisha ya familia yangu. Napaswa kuwafahamu ili niwafundishe vizuri. Hiyo ni sawa, napaswa kuwa mtu ninaye “umuhimu” wa kuhubiri na kufundisha! Kwamba “umuhimu” sio tu kwa wakubwa pekee. Au “umuhimu” hu ni juu ya wahubiri pekee. Napaswa kuhisi umuhimu wa majukumu ambayo nimepewa. Napaswa kuwa tayari kuendana na kauli ya Paulo, “*...ole wangu nisipoihubiri injili.*” (1 Kor. 6:16)! Je itachukua jukumu? Je itachukua muda? Ndio! Ikiwa tu nafsi moja itakimbia adhabu ya moto, basi juhudi zote zitakuwa na thamani.

Hivyo, unafanya nini leo? Je utakaa kimya kuhusu injili? Je utasema kwamba hujasoma vizuri na siwezi kumfundisha mtu ye yote. Je utapata idadi yoyote ya udhuru ambazo hazitoshi? Labda, msomaji wa kipeperushi hiki atakuwa mkali katika changamoto. Labda, ni labda tu, msomaji huyo ni wewe. Kila mtu na akumbuke kwamba mtu fulani, kwa wakati fulani, anapaswa kuwa mtu aliyetufundisha, kama mtu aliyekuja kutoka Marekani alivyofungua akili zetu. Vipi kama wasingeona “umuhimu” wa kumtuma Africa? Tutakuwa wapi Kiroho?